




# UMOJA
# UN Tanzania

**Toleo Na. 81**
**Novemba- Desemba 2018**


## Ujerumani yasaidia kazi za kutoa misaada ya kibinadamu kwa wakimbizi zinazofanywa na WFP nchini Tanzania



Mchango wa Euro milioni 3.25 kutoka Ujerumani kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) utatoa msaada unaookoa uhai kwa zaidi ya wakimbizi 290,000 ambao hivi sasa wamepewa hifadhi katika Mkoa wa Kigoma. ***Picha | WFP/Tala Loubieh***

### Vidokezo

- Mchango wa wanaojitolea katika kujenga jamii himilivu yatambuliwa katika Siku ya Kimataifa ya Wanaojitolea (IVD)
- RIPOTI MAALUMU: Siku 16 za Harakati dhidi ya Vitendo vya Ukatili kwa Msingi wa Jinsia
- Vijana wapaaza sauti katika maadhimisho ya Siku ya Watoto Duniani jijini Dar es Salaam

Mwezi Desemba, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) lilipokea mchango wa Euro milioni 3.25 ukiwa ni mchango kutoka katika Jamhuri ya Kifederali ya Ujerumani ili kusaidia kazi za shirika hilo za kusaidia wakimbizi na wanaotafuta hifadhi nchini Tanzania kwa mwaka 2018-2019.

“WFP inashukuru mno kwa mchango huu mkubwa kutoka Serikali ya Watu wa Ujerumani,” alisema Mwakilishi wa Nchi wa WFP Tanzania, Bw. Michael Dunford, “Ujerumani imeendelea kuwa mshirika muhimu katika uendeshaji programu za WFP ambapo misaada yake ni ya kutoa chakula ili kuokoa uhai wa wakimbizi waliopata hifadhi Tanzania.”

WFP hutoa migao ya chakula kila mwezi ikihusisha nafaka, kunde, mafuta yatokanayo na mimea na chumvi na pia vyakula vilivyorutubishwa kwa ajili ya akina mama wajawazito na wanaonyonyesha walio hatarini, watoto wa umri wa chini ya miaka mitano, watu wenye utapiamlo wanaoishi na VVU/UKIMWI na wagonjwa waliolazwa. Zaidi ya hayo, biskuti zenye kutoa nguvu kubwa pia hugawiwa kwa wakimbizi walio katika vituo vya mpito.

Tanzania imetoa hifadhi kwa zaidi ya wakimbizi 290,000, wengi wao

*Inaendelea ukurasa wa 2*

## Kauli ya Serikali

***“…nawashukuru Wadau wa Maendeleo waliounga mkono na kuweza kufanikisha Kampeni hii. Kwa hakika sitaweza kumtaja kila mmoja lakini naomba niwataje wafuatao: Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Wanawake (UN-Women); Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Elimu, Sayansi, na Utamaduni (UNESCO)…”***

**Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa, akizungumza katika uzinduzi wa maadhimisho ya siku 16 za kupinga unyanyasaji wa kijinsia yaliyofanyika mjini Dodoma tarehe 25 Novemba, 2018.**

Jarida hili linachapishwa na Kitengo cha Mawasiliano cha UN nchini Tanzania. Kujisajili na kutoa mrejesho, tafadhali wasiliana nasi kupitia: hoyce.temu@one.un.org. Tovuti: www.tz.one.un.org Simu: (+255) 22-219-5021

*Inatoa ukurasa wa 1*

wakiwemo wanawake na watoto katika Kambi za Wakimbizi za Nduta, Nyarugusu na Mtendeli zilizo katika Mkoa wa Kigoma, kaskazini magharibi mwa Tanzania. Zaidi ya asilimia 70 ya wakimbizi wanatoka nchini Burundi, na waliobaki wanatoka katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo.

“Nchi yangu inajivunia kuisaidia WFP ili nayo iwasaidie wale wanaokimbilia Tanzania ili kujiokoa,” alisema Dkt. Detlef Waechter, Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania. “Itakuwa muhimu sana kuhakikisha hali ya kisiasa nchini mwao inakaa sawa kabla wakimbizi hawajarejea makwao kwa hiyari na usalama.”

Ingawa ukosefu wa fedha ulilazimisha migao ya chakula kupunguzwa kati ya Februari, 2017 na Oktoba, 2018, kuongezeka kwa misaada kutoka kwa wafadhili, ikiwemo Ujerumani, kumewezeshwa kiwango cha awali cha migao kuanza kutolewa tena. WFP inaendelea na harambee za kukusanya fedha ili migao ya chakula cha wakimbizi isipunguzwe katika miezi ijayo.

## Mchango wa wanaojitolea katika kujenga jamii himilivu yatambuliwa katika Siku ya Kimataifa ya Wanaojitolea (IVD)



Wanachama wa Chama cha Kujitolea cha UN wakiwa na Mratibu Mkazi, Bw. Alvaro Rodriguez na Balozi Ali Karume, Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo (walioketi, katikati kushoto) wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanaojitolea huko Zanzibar. ***Picha | UN Volunteers***

Siku ya Kimataifa ya Wanaojitolea (IVD) ilipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1985. Tangu wakati huo, kila mwaka serikali mbalimbali, mfumo wa UN na vyama vya kiraia wamefaulu kuungana na wanaojitolea kote duniani ili kusherehekea Siku hiyo inayoadhimishwa kila Desemba 5. Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanaojitolea (UNV), zaidi ya watu bilioni moja kote duniani wanajitolea, hii ni sawa na kazi ya watu milioni 109 walio katika ajira ya kudumu. Wengi kati ya wale wanaojitolea wanafanya kazi nje ya utaratibu wa kawaida, huku takribani asilimia 70 ya wanaojitolea wakifanya hivyo katika jamii zao wakiwasaidia majirani zao, ambapo asilimia 30 ya wanaojitolea wanafanya hivyo katika mashirika rasmi. Katika IVD 2018, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Mataifa waliadhimisha jamii ya wanaojitolea wanaozisaidia jamii zao kuwa himilivu zaidi dhidi ya majanga ya asili, hali ngumu ya kiuchumi na mitikisiko ya kisiasa.

Sherehe zilifanyika huko Zanzibar na ziliratibiwa na UNV kwa kushirikiana na mashirika 10 mengine ya wanaojitolea. Maadhimisho hayo yalifanyika katika Viwanja vya Mapinduzi na kuwaleta pamoja wanaojitolea takribani 300. Takribani chupa 250 za damu zilipatikana na kukabidhiwa kwa Benki ya Taifa ya Damu, ambayo imekuwa ikikabiliana na changamoto za kukosa kuvutia kwa wingi wanaojitolea damu. Mgeni rasmi katika tukio hilo alikuwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Ali Karume, na Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez.







Wanachama wa Chama cha Kujitolea cha UN wakijitolea damu na kushiriki katika huduma mbalimbali za afya katika Viwanja vya Mapinduzi huko Zanzibar wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kujitolea. ***Picha | UN Volunteers***

# Mkuu wa operesheni za UN za kulinda amani atoa heshima kwa vikosi vya Tanzania huko Zanzibar



Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia Operesheni za Kulinda Usalama, Bw. Jean Pierre Lacroix akikutana na wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hapa akisalimiana na Brigedia Jenerali Nondo (pia mkuu wa Brigedi ya 1010), wakati wa tukio la Gwaride la Heshima. ***Picha | UN***

Mwaka mmoja tangu yatokee mauaji ya kutisha ya walinda amani 15 wa Umoja wa Mataifa kutoka Tanzania huko Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, kiongozi wa Shughuli za Kulinda Amani (DPKO) alizitembelea familia za waathirika mwezi uliopita ili kutoa heshima kwa askari hao waliouwawa katika kile kinachoonekana kuwa pigo kubwa kwa Walinda Amani wa UN katika historia ya hivi karibuni.

Akizungumza huko Visiwani Zanzibar, ambako ndiko walikotoka walinda amani 13 kati ya 15 waliouwawa, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Jean-Pierre Lacroix aliwaambia familia za waathirika wa mauaji hayo kwamba wapendwa wao na sadaka zao hazitakaa zisahaulike kamwe.

“Najua ni jambo gumu sana na hakuna maneno ya kutosha kuelezea uchungu wenu. Lakini, naomba niwahakikishie, kwamba kamwe hamtawasahau mashujaa wenu hao, na sisi pia hatutawasahau kamwe,” alisema.

Hotuba ya mkuu wa ulinzi wa amani ilihitimisha ziara ya siku mbili nchini Tanzania, ambapo alikutana pia na wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mnamo Desemba 7, 2017, wanaohisiwa kuwa wapiganaji wa Kikundi cha Allied Democratic Force (ADF), walikivizia kikosi cha Kulinda Amani cha Umoja wa Mataifa nchini DRC (MONUSCO), katika Kambi yake ya Operesheni huko Semuliki katika Mkoa wa

***Inaendelea ukurasa wa 4***



Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia Operesheni za Kulinda Usalama, Bw. Jean Pierre Lacroix (katikati), na Mwakilishi Maalumu na Mkuu wa Misheni ya Kulinda Amani katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (MONUSCO), Bi. Leila Zerrougui (kulia), wakiwafariji wanafamilia waliopoteza wapendwa wao katika misheni ya kulinda amani huko Kongo mwaka jana. ***Picha | UN***

*Inatoka ukurasa wa 3*

Beni, Jimbo la Kivu Kaskazini. Mapigano makali yalitokea yakihusisha waasi, walinda amani wa UN, na vikosi vya Serikali.

Licha ya walinda amani 15 wa kutoka Tanzania waliotumikia kikosi cha UN waliouwawa, 44 wengine walijeruhiwa.

Jimbo la Kivu Kaskazini huko Mashariki mwa DRC, limekuwa eneo tete kwa vikosi vya kulinda amani vya Umoja wa Mataifa. Miezi miwili kabla ya mashambulizi hayo ya waasi ya mwezi Desemba, askari wawili wa kulinda amani waliuwawa na wengine 18 kujeruhiwa katika shambulizi lililotokea katika eneo hilo hilo.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa António Guterres aliyaita mauaji ya Desemba 7 kama ishara ya kuongezeka kwa changamoto zinazokabili operesheni za UN za kulinda amani kote duniani, na katika hotuba yake mara baada ya shambulizi, alisema kwamba vitendo hivyo vya makusudi "havikubaliki" na ni "uhalifu wa kivita".

Katika mwaka 2017, zaidi ya walinda amani 110,000 walitumwa katika maeneo 15 yenye hatari kote duniani, na karibu watumishi 19,000 wa UN wanafanya kazi nchini DRC peke yake, jambo linaloifanya nchi hiyo kuwa eneo la pili kubwa zaidi nyuma ya UNMISS kule Sudani ya Kusini.

Tangu mwaka 2010, walinda amani 154 wameuwawa nchini DRC.

## Vikundi vya akiba vyaleta matumaini kwa wakimbizi wanawake




Nadia, mwananchama wa kikundi cha akiba kinachosaidiwa na UNCDF, akijiandaa kwa ajili ya siku yenye shughuli nyingi katika Kambi ya Nyarugusu. ***Picha | UNCDF***

"Hivi sasa familia yangu inanisikiliza," alisema Ekyoci, mwanamke raia wa Kongo mwenye umri wa miaka 34. "Kila mara ninapokuwa na mchango wa mawazo, kama kufanya marekebisho kwenye nyumba na jinsi ya kutumia fedha zetu, mume wangu ananisikiliza. Haikuwa hivyo hapo kabla."

Ekyoci ni mkimbizi ambaye ameishi katika Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu kwa miaka 22. Tangu alipowasili, Ekyoci amekua kutoka binti mdogo hadi kuwa mama wa

*Inaendelea ukurasa wa 5*

*Inatoka ukurasa wa 4*

watoto watatu, lakini kwa mujibu wake, bado hakuna dalili za amani ya kudumu nyumbani.

Hivi sasa Ekyoci anaendesha biashara yake ndogo ambapo yeye hununua mbogamboga kutoka katika jamii za wenyeji na kuziuza katika soko la wazi la kambini hapo. Biashara hiyo inamwingizia takribani Tsh12,000 ($5.20) kama faida kwa mwezi, ambayo yeye huiweka akiba katika kikundi cha akiba kinachofadhiliwa na UNCDF. "Kabla ya kujiunga na kikundi hiki, nilitumia kila senti niliyopokea," alisema Ekyoci. Ukosefu wa ujuzi ulimkwamisha katika namna ya kupanga na kusimamia fedha zake. "Kingine kilichobadilika ni mtazamo katika famila—sasa wanaheshimu maoni yangu, kwa sababu ninafanya biashara na kuchangia kipato katika kaya."




Wanachama wa vikundi vya akiba vinavyosaidiwa na UNCDF wakiuza bidhaa zao katika Soko la Pamoja la Nyarugusu. ***Picha | UNCDF***

> *Kingine kilichobadilika ni mtazamo katika famila—sasa wanaheshimu maoni yangu, kwa sababu ninafanya biashara na kuchangia kipato katika kaya."*
>
> **- Ekyoci, mwanamke raia wa Kongo mwenye umri wa miaka 34**

Licha ya kukabiliwa na vikwazo kadhaa, Ekyoci ni mfano mzuri wa jinsi vikundi vya kujiwekea akiba vinavyomjengea mtu tabia ya kuweka akiba, kujenga kujiamini, na kuwawezesha wanawake katika ngazi ya mtu binafsi na ile ya jamii.

Muundo wa kikundi cha kuweka akiba wa UNCDF unatoa fursa kwa kaya za kipato cha chini kujipatia mali; kuleta utayari wa kukabiliana na dharura, magonjwa, au majeraha; na kufanya uwekezaji wenye tija.

Juhudi kama hizo za kujitafutia riziki ndizo zinazoimarisha uwezo wa wakimbizi kujijengea uwezo wa kujitegemea na kuimarisha uelewa wetu kuhusu watu wanaotafuta migao ya chakula—hasa pale wanapopatiwa zana na fursa sahihi, kwamba mikono hii inaweza kujijengea njia ya kuhimili na kukuza kipawa ambacho kimetikiswa na migogoro na kuondolewa nchini kwao.

Kwa maelfu ya wanawake walio wanachama katika vikundi vya akiba vinavyosaidiwa na UNCDF, mkopo mmoja unatosha kujenga maisha ya baadaye, kwa kutoa fursa ya maisha yenye dira na matumaini.

# RIPOTI MAALUMU
## Siku 16 za Harakati dhidi ya Vitendo vya Ukatili kwa Msingi wa Jinsia



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa (kulia) na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mh. Ummy Mwalimu (kushoto) wakiwa katika uzinduzi wa Kampeni ya Siku 16 ya Uanaharakati wa Kupinga Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia. Kampeni ilizindliwa katika Viwanja vya Jamhuri, Dodoma. ***Picha | Zainul Mzige***

Nchini Tanzania, vita dhidi ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana imekuwa ndiyo mtindo wa maisha si kwa polisi peke yao bali katika mahakama kwa ajili ya wanaume kama zile zinazopatikana mkoani Kigoma.

Kwa mujibu wa Bw. Yassin Ally, mkurugenzi mtendaji wa Kikundi cha Kutetea Haki za Mwanamke cha Kivulini cha Mkoa wa Kigoma, vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana vimepitwa na wakati, na ni vya kufedhehesha hasa katika baadhi ya ofisi katika maeneo ambayo yamestaarabika. Shirika lake linaingia katika makubaliano na UN Women katika miradi inayolenga kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana.

Kigoma ni miongoni mwa mikoa iliyochaguliwa mwaka huu kwa ajili ya kampeni za Siku 16 za Harakati Dhidi ya Vitendo vya Ukatili kwa kutumia kampeni ya kuongeza kasi ya jitihada za kuwalinda wanawake na wasichana na kuwezesha uanzishwaji wa jamii zenye amani.

Jumla ya asilimia 61 ya wanawake, wenye umri kati ya miaka 15-49, wamewahi kunyanyaswa kwa vitendo vya ukatili vya kingono, au kihisia vinavyofanywa na waume au wenza wao; ambapo asilimia 33.4 wanateswa na vitendo vya ukatili; ambapo asilimia 33.4 walitendewa vitendo vya ukatili ndani ya miezi 12 kabla ya utafiti wa Kidemografia na Afya wa 2015/16.

Ni kutokana na ufadhili mnono kutoka Serikali za Norway na Sweden, mwezi Aprili 2018, Kikundi cha Haki za Wanawake cha Kivulini kilianza kutekeleza miradi ya mwaka mmoja ya Kasulu, Kakonko na Kibondo.

Juhudi hiyo inalenga kujenga uwezo wa jamii wa kutoa mwitikio kwa vitendo vya ukatili. Baada ya miezi kadhaa ya kufanya kazi na wanajamii na jamii ya mahalia, Ally alisema mitazamo ya watu inaanza kubadilika, ambapo baadhi ya wanaume nao pia wanajitolea kama mashujaa wa utetezi wa amani.

"Tumeanza kuona baadhi ya mabadiliko. Mashujaa wanaume sasa wanachukulia ukatili dhidi ya wanawake na wasichana kama usaliti kwa familia zao na nia ya nchi ya kulinda haki za wanawake. Sasa wanaamini kwamba kila mwanamke anastahili kuishi kikamilifu na kwa amani," alisema Ally.

Kufuatia ushirika na Shirika la UN la Wanawake (UN Women), takribani watu wanaojitolea 300, wakiwemo wanaharakati 50 wamepata

*Inaendelea ukurasa wa 7*

*Inatoka ukurasa wa 6*
mafunzo yaliyowawezesha kuwa mashujaa wa kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Kampeni iliyofanyika Kigoma pia inawalenga polisi, watendaji wa serikali za mitaa, watumishi wa sekta ya afya, waalimu na maofisa wa mahakama katika juhudi zinazoendelea za kuishirikisha jamii kwa malengo ya kuimarisha utoaji huduma.

Kwa namna ya pekee, kampeni ya Siku 16, ilitoa ujumbe wa wazi kwamba hata wanaume walio katika nyadhifa za juu nao pia ni sehemu ya mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Kampeni ilizinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa, na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi huko Zanzibar, ni ushahidi unaoonyesha utayari wa serikali katika suala hili.

Akizungumza wakati wa Siku 16 huko Zanzibar, Mwakilishi wa UN Women nchini Tanzania, Hodan Addou alikaribisha ushiriki wa maofisa wa ngazi za juu wa serikali; UN; vyama vya kiraia; sekta binafsi; jamii za mahalia katika shughuli zote muhimu. Alieleza kwamba hii ilidhihirisha umuhimu wa kuendelea kupigania usawa wa jinsia katika sekta zote, yaani ili kuiwezesha Tanzania kupiga hatua za maana katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

"Ninaamini katika ushirika ulio imara ndiyo tunaweza kuongeza ubora katika maisha ya wanawake na wasichana wengi nchini Tanzania. Jambo hili ni muhimu kwani kufanikiwa kwa wanawake na wasichana ndiyo kufanikiwa kwa Tanzania," alisema Addou.

Alisisitiza umuhimu wa kutengeneza mazingira wezeshi zaidi, pasipo na unyanyasaji, sambamba na kuwekeza katika elimu ya wasichana na juhudi zaidi za maendeleo kwa wanawake wote ili kuwezesha ushiriki wao kamili katika maendeleo ya nchi.

> *"Ninaamini katika ushirika ulio imara ndiyo tunaweza kuongeza ubora katika maisha ya wanawake na wasichana wengi nchini Tanzania. Jambo hili ni muhimu kwani kufanikiwa kwa wanawake na wasichana ndiyo kufanikiwa kwa Tanzania,"*
>
> **- Hodan Addou, Mwakilishi wa UN Women nchini Tanzania**




Kiongozi wa Shirika la UN la Wanawake (UN Women) katika kupambana na Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia, Haki za Binadamu na VVU/UKIMWI, Bi. Lucy Tesha (kushoto) akiwa na wavulana kutoka Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma, wakati wa maadhimisho ya Kampeni ya Siku 16 huko Kigoma. Kampeni ya Siku 16 mkoani humo ni sehemu ya Programu Kamambe ya Pamoja ya Mkoa wa Kigoma (KJP). ***Picha | Zainul Mzige***



(Mstari wa mbele, kutoka kushoto) Mkurugenzi wa Nchi wa UNAIDS, Dkt. Leo Zekeng; Mwakilishi wa UN Women, Bi. Hodan Addou; na Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez, pamoja na maofisa wengine wa UN, wakiwa katika mzunguko wa barabara wa Jamatini, Dodoma. UN Women ilipamba mzunguko huo kwa rangi za machungwa ikiwa ni sehemu ya Kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati wa Kupinga Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia. ***Picha| Zainul Mzige***




Mwanamuziki Christina Shusho akitumbuiza kwa wimbo kuhusu kukomeshwa kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Siku 16 huko Dodoma. ***Picha | Zainul Mzige***

# Vijana wapaza sauti katika maadhimisho ya Siku ya Watoto Duniani jijini Dar es Salaam




Waziri Ummy Mwalimu alikuwa mgeni rasmi katika Mazungumzo Motomoto (Activate Talk) na alirudia ahadi ya serikali ya kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya watoto nchini. ***Picha | UNICEF***

> *"Kizazi kijacho kitakuwa ni kizazi cha vipaji na wagunduzi katika dunia inayobadilika kwa kasi sana. Wanachokihitaji ni fursa – ya kusikilizwa na kuungwa mkono katika kufanya uchaguzi sahihi ili wakue wakiwa na matumaini na maisha yenye umotomoto, malengo na huruma,"*
>
> **- Ms. Maniza Zaman , Mwakilishi wa UNICEF.**

Vijana wapaza sauti zao katika maadhimisho ya Siku ya Watoto jijini Dar es Salaam. Mwishoni mwa mwezi Novemba, UNICEF Tanzania, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliandaa Mazungumzo Motomoto (Activate Talk) na watoto na vijana kuhusu ujumbe wa "Ndoto Zangu, Njia Yangu …" ili kuadhimisha Siku ya Watoto Duniani.


Mgeni Rasmi katika tukio hilo alikuwa ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mh. Ummy Mwalimu, lakini pia lilihudhuriwa na watoto, maofisa wa serikali, Wabunge, washirika wa maendeleo, viongozi wa dini na sekta binafsi.

Lengo lilikuwa kuwapa vijana nafasi ya kutiwa moyo, kuhamasishwa na kuhimizwa kufuatilia ndoto zao na kubaki na matumaini kwa maisha ya baadaye, licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali.

Vijana watano walielezea uzoefu wao jinsi walivyofaulu kudumu katika kufuatilia ndoto na matamanio yao licha ya kukabiliana na changamoto mbalimbali.

Wazungumzaji hao walikuwa ni Mlimbwende wa Tanzania kwa mwaka 2012 Brigitte Lyimo; mwanafunzi mwenye miaka 14 Vanessa Innocent; mtangazaji wa redio Millard Ayo; mwanafunzi

***Inaendelea ukurasa wa 10***



Mazungumzo Motomoto yalibeba ujumbe uliohusu mada, "Ndoto Zangu, Njia yangu ya Kuhamasisha Vijana kote nchini ili kufuata ndoto licha ya changamoto zinazoweza kujitokeza katika safari yao ya maisha. ***Picha | UNICEF***

*Inatoka ukurasa wa 9*

wa chuo kikuu wa Uhandisi wa Kompyuta, Witness Mtui; na kiongozi wa Baraza Dogo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Raphael Dennis. Sauti zao ziliwatia moyo wenzao na kuamsha mazungumzo yenye tija kati ya vijana na wadau wengine kuhusu jinsi wanavyoweza kuhakikisha watoto nchini Tanzania wanakua wakiwa wenye matumani na hatma yao.

Moja ya ujumbe mkuu katika mazungumzo hayo ilikuwa vijana kuwa huru na kuchagua kile ambacho wangependa wawe, hasa kuhusiana na uchaguzi wa kazi watakazofanya, na kuelezea matamanio yao kwa wazazi huku familia zikiwaunga mkono katika kufanikisha ndoto zao hizo.

Katika hotuba yake, Bi. Mwalimu, aliwakumbusha wazazi kushiriki kikamilifu katika makuzi ya watoto wao huku akirejelea utayari wa serikali kukomesha vitendo vya ukatili dhdi ya watoto nchini.

Mwakilishi wa UNICEF, Bi. Maniza Zaman, alisema kwamba vijana raia wa leo, watakuwa na mchango muhimu katika kuhakikisha utekelezaji wa hatua zilizopitishwa kwa ahadi iliyotolewa kupitia SDGs na kwamba haya yatakuwa na athari kubwa zaidi kwao.

“Kizazi kijacho kitakuwa ni kizazi cha vipaji na wagunduzi katika dunia inayobadilika kwa kasi sana. Wanachokihitaji ni fursa – ya kusikilizwa na kuungwa mkono katika kufanya uchaguzi sahihi ili wakue wakiwa na matumaini na maisha yenye umotomoto, malengo na huruma,” alieleza Bi. Zaman.




Watoto na vijana kote nchini kutumia #GoBlue kijiunga na UNICEF Tanzania katika Mazungumza Motomoto katika Siku ya Watoto Duniani. Vijana, watoto na #ChangeMakers walishiriki kikamilifu kuwatia moyo vijana wa Tanzania kutimiza ndoto na matamanio yao. ***Picha| UNICEF***

## Miradi ya kujitafutia riziki yagusa maisha ya Watanzania na Warundi



Wanufaika wa bustani za nyumbani wakihudumia bustani hizo kwa usimamizi wa Bw. Sinzikayo. ***Picha | UNHCR/Winnie Kweka***

Akiwa ameamka saa 12 asubuhi, Bw. Sinzikayo anahudumia mbogamboga katika bustani yake ndogo kabla ya kuelekea katika kazi yake ya kutwa katika shirika la Good Neighbours Tanzania (GNTZ), ambalo ni mshirika wa UNHCR katika Mkoa wa Kigoma. Bw. Sinzikayo (50) ana shahada ya kwanza katika kilimo na mifugo kutoka Chuo Kikuu cha Burundi na ana zaidi ya miaka 10 ya uzoefu, anaishi katika Kambi ya Wakimbizi ya Mtendeli.

Mapenzi na kazi yake katika kilimo yana mchango wa moja kwa moja kwa zaidi ya wakimbizi 170 na wenyeji zaidi ya 240 katika jamii inayoishi jirani na kambi hiyo

*Inaendelea ukurasa wa 11*

*Inatoka ukurasa wa 10*
ambao sasa wanaweza kupata mlo kamili na pia kujiongezea kipato. “Nilikimbilia Tanzania ili kupata maisha bora kwa familia yangu mwaka 2016 baada ya kuona miili ya marafiki zangu ikielea mtoni huko nyumbani,” alisimulia Bw. Sinzikayo.

Mwaka mmoja baadaye, alijiunga na programu ya kilimo ya GNTZ na anatumia ujuzi wake kuwafundisha wakulima wadogo Warundi na Watanzania wanaolima kwa kutumia njia za kilimo hai. Kupitia programu hii, Bw. Sinzikayo amejikita katika kuwafundisha wanufaika namna ya kulima mbogamboga kama vile kabichi, spinachi, pilipili hoho, vitunguu na pilipili kwa matumizi ya kujikimu na kuuza.

“Bw. Sinzikayo ni mwalimu hodari ambaye hututia moyo tuulize maswali naye hufundisha kwa vitendo,” alisema Donasien, mwanakijiji kutoka Kasanda jirani na Kambi ya Mtendeli. “Mwalimu wetu bado anatembelea bustani yangu iliyo nje ya jiko ili kuona namna gani pilipili hoho na karoti zangu zinavyokua,” alisema Marina, mkimbizi Mrundi na mama wa watoto wawili.

“Kwa kweli yeye ana ujuzi mwingi sana katika eneo hilo, Bw. Sinzikayo angeweza kuendesha mradi mkubwa wa kilimo, ikiwa tu hali ingalikuwa tofauti,” alieleza Takaaki Miura, Ofisa Mwandamizi wa Njia za Kujikimu wa UNHCR. “Kilimo ndiyo sekta inayotawala katika Mkoa wa Kigoma na hata Burundi, tungependa kuona ubadilishanaji wa maarifa kama haya kati ya pande hizi mbili za mpaka,” aliongeza Takaaki.

Bw. Sinzikayo anafurahia kazi yake na anatamani kwamba mambo mengi zaidi yangefanywa ili kupanua miradi ya kilimo. “Natamani kwamba tungepanua ili kutoa mafunzo ya ufugaji mifugo ili kuongezea katika yale mafunzo ya uendeshaji bustani ndogondogo, na vifaa zaidi ya kilimo,” aliongeza. Ameoa na ana watoto watano.



Bw. Sinzikayo akiwa katika bustani yake ya nyumbani. ***Picha| UNHCR/ Winnie Kweka***

## UNDP yasaidia upatikanaji wa misaada ya kisheria kote Tanzania

Ili kuendeleza mafanikio ya miaka iliyopita, Wizara ya Katiba na Mambo ya Sheria, kwa kushirikiana na UNDP Tanzania na Mtandao wa Wasaidizi wa Sheria Tanzania (TAPANET), iliandaa na kuratibu Wiki ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2018 kuanzia Novemba 26 hadi Novemba 30, 2018.

Wiki ya Msaada wa Kisheria ilizinduliwa na Wizara huko Morogoro wiki ya mwisho ya Novemba ili kutambua ukweli kwamba kuna mamilioni ya wakazi nchini Tanzania ambao fursa yao ya kupata maarifa kuhusu namna ya kupata msaada wa kisheria ni ndogo. Kupitia mradi wa Kuimarisha Upatikanaji wa Haki na Kinga ya Haki za Binadamu, UNDP inaisaidia Wizara ya Katiba na Mambo ya Sheria kuimarisha usimamizi wa sekta ya msaada

*Inaendelea ukurasa wa 12*



Shughuli za Wiki ya Msaada wa Kisheria zikiendelea huko wilayani Kasulu. Huduma za msaada wa kisheria zilitolewa zaidi na wasaidizi wa mambo ya sheria, polisi kutoka Dawati la Jinsia, wanasheria, Wanasheria wa Serikali na Mawakili. ***Picha | UNDP***

***Inatoka ukurasa wa 11***

wa kisheria kupitia utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya 2017, na kusaidia juhudi ambazo zinasaidia kueneza upatikanaji wa msaada wa kisheria.

Wanawake na wasichana hawapati fursa kamili na kwa hiyo, ujumbe katika Wiki ya Msaada wa Kisheria kwa mwaka huu ilikuwa 'Usawa katika kupata msaada wa kisheria kwa Wanawake na Wasichana wote'. Matukio kote nchini yalitoa elimu, ushauri na msaada wa kisheria kwa takribani wahitaji 500,000 na watu walio hatarini (takwimu za awali). Huduma za msaada wa kisheria zilitolewa na wanasheria wasaidizi kutoka TAPANET, mawakili, polisi kutoka Dawati la Jinsia, na wanasheria wa serikali.

Tukio hilo ni mfano mzuri wa namna ya kuhakikisha upatikanaji wa msaada wa kisheria unavyohitaji ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika sekta ya sheria; serikali za mitaa na serikali kuu; na vyama vya kijamii. Umuhimu wa msaada wa kisheria Tanzania ulisisitizwa zaidi wakati wa maadhimio ya kumbukumbu ya Miaka 20 ya Tamko la Walinzi wa Haki za Binadamu mnamo Desemba 9 (Siku ya Walinzi wa Haki za Binadamu), tukio ambalo liliandaliwa na Shirikisho la Walinda Haki za Binadamu (HRDC) na Mtandao wa Wataalamu wa Msaada wa Sheria (TANLAP), ambalo kwalo UNDP ilishiriki.



Wakati wa Wiki ya Msaada wa Kisheria katika Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma, jumla ya watu 294 walihudumiwa na miongoni mwao 154 walikuwa wanawake. ***Picha | UNDP***

## Ripoti ya UNCTAD ya Nchi Zinazoendelea yazinduliwa




Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD). ***Picha | Maktaba***

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo ilizinduliwa mnamo Novemba 22 katika Ofisi za ILO, jijini Dar es Salaam na Ofisa wa Masuala ya Uchumi wa UNCTAD, Bw. Dennis Banda na Bi Ellen Maduhu kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mratibu wa UN Tanzania, Bw. Alvaro Rodriguez.

Kichwa kidogo cha ripoti hiyo ya 2018 kilikuwa: "Ujasiriamali kwa Mageuzi: Zaidi ya Kufanya Mambo Kikawaida". Wanadiplomasia, watafiti, wawakilishi wa vyombo vya habari na maofisa wa UN walishiriki katika uzinduzi huo.

Ripoti ilipima hali ya ujasiriamali katika Nchi Zinazoendelea (Nchi Changa), ambapo iliona kwamba miongoni mwa mambo ambayo wajasiriamali wanaweka mkazo ni biashara za kiwango cha kati na wanakosa ujasiri wa kuvumbua ambayo ni tabia inayofanya biashara hizo kutodumu. Ripoti hii pia ilionyesha mchango wa wajasiriamali katika maendeleo ya nchi changa katika kupiga hatua kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) jambo lililoashiria kwamba zingeweza kufanyiwa mageuzi ili kuleta ubunifu zaidi na kuchangia zaidi katika upatikanaji wa haraka zaidi wa malengo.

Ripoti ilitoa hoja kwamba mageuzi ya kimuundo yanahitaji kufanyika ili kuwajumuisha wajasirimali wa mahalia katika mnyororo wa thamani wa dunia ili kuwafanya wawe na tija zaidi.

Changamoto wanazozikabili wajasiriamali ziliainishwa na mapendekezo kutolewa. Kwa mfano, moja ya mapendekezo ilikuwa kwamba sera hazina budi kulenga makampuni yanayozingatia zaidi mabadiliko – yale yaliyo na uwezekano mkubwa zaidi wa kuondoa ukosefu wa tija katika uchumi wa nchi changa na kuongeza uzalishaji, na wakati huo huo kutengeneza ajira zaidi na kuweza kudumu katika soko la dunia la sasa. Ripoti inaainisha aina ya sera zinazofaa zaidi ili kusukuma ujasiriamali wa kimageuzi.

Ripoti ya UNCTAD ya Nchi Changa inatoa chanzo kamilifu na chenye mamlaka kwa uchambuzi wa data za kijamii na kiuchumi. Ripoti imekusudiwa kutumiwa na watumishi wa serikali, watunga sera na wote wale wanaohusiana na sera za maendeleo ya nchi changa.

# Siku ya Kimataifa ya Wahamiaji Tanzania, 2018




Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mh. Mhandisi Hamadi Masauni, alikuwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wahamiaji Duniani. Alizungumzia jitihada za Wizara ya Mambo ya Ndani za kuongeza ubora wa huduma za uhamiaji na kuwahimiza wazazi kuwalinda watoto wao dhidi ya watu wanaojihusisha na biashara haramu ya binadamu. ***Picha | IOM***

Shirika la Umoja wa Mataifa la Wahamiaji -- International Organization for Migration (IOM) – liliiungana na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wahamiaji mnamo Desemba 18, 2018 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam. Ujumbe wa mwaka huu ulikua “Uhamiaji wenye Hadhi”.

Maadhimisho ya 2018 ya Siku ya Kimataifa ya Wahamiaji yalianza tangu Desemba 16 hadi Desemba 18. Siku mbili za mwanzo zilitumiwa kutoa elimu ya uraia na taarifa kwa wageni waliofika kwenye maonyesho. Hizi zilikuwa ni pamoja na huduma zinazohusiana na uhamiaji kama vile hati za kusafiria za kielektroniki na visa za kielektroniki, miongoni mwa mambo mengine. Zaidi ya hayo, mabanda ya maonyesho yalijengwa kama sehemu ya maadhimisho na yalionyesha kazi za IOM Tanzania, Idara ya Uhamiaji Tanzania na Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda cha Mjini Moshi ambacho kinaendeshwa kwa ushirikiano na Kituo cha IOM cha Afrika cha Kujenga Uwezo.

Katika Siku ya Wahamiaji yenyewe, Desemba 18, 2018 – serikali ya Jamhuri ya Muungano

***Inaendelea ukurasa wa 15***




Hotuba ya Siku ya Wahamiaji Duniani ya mwaka 2018 kutoka kwa Dkt Anna Makakala-Kamishna Jenerali wa Idara ya Uhamiaji. ***Picha | IOM***

*Inatoka ukurasa wa 14*

wa Tanzania kupitia Idara ya Huduma za Uhamiaji, iliongoza tukio la siku kwa kusaidiwa na IOM Tanzania.

Mgeni Rasmi alikuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamadi Masauni. Siku ya maadhimisho ilihudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwemo wawakilishi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya serikali, Katibu Mkuu wa Sekretariati ya Kupambana na Biashara Haramu ya Kusafirisha Binadamu Tanzania na wananchi kwa ujumla.




Ofisa Uhamiaji Salma Panja kutoka Chuo cha Mafunzo ya Uhamiaji cha Kikanda cha Nchini Tanzania akizungumza kuhusu ushirika wa Chuo hicho na Kituo cha Kujenga Uwezo cha Afrika. ***Picha | IOM***

Mgeni Rasmi alizungumzia juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha huduma za uhamiaji kupitia Idara ya Uhamiaji kwa kuanzisha uhamiaji wa kielektroniki, visa za kielektroniki na vibali vya kielektroniki kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ambazo zinashughulikia changamoto za usimamizi wa uhamiaji nchini.

Pia aliangazia umuhimu wa wahamiaji kuzingatia taratibu rasmi na sheria za nchi pale wanapoingia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwahimiza wazazi na walezi kuwatunza watoto/vijana wao ili wasiangukie katika mikono ya wasafirishaji haramu wa binadamu wanaowashawishi kwenda nje kwa ahadi ya kuwatafutia kazi.

## Zaidi ya Vijana 600 Wapata Mafunzo kuhusu Malengo ya Dunia huko Unguja na Pemba




UNICEF yafanikisha mafunzo ya Malengo ya Dunia kwa zaidi ya vijan 200 Unguja. ***Picha | UN***

Umoja wa Mataifa nchini Tanzania unaendelea kutoa elimu kuhusu Malengo ya Dunia. Hivi karibuni, kwa ufadhili wa UNICEF, Umoja wa Mataifa Tanzania ulitoa mafunzo na kuendesha mijadala ya moja kwa moja na zaidi ya vijana 600 ili kuwawezesha kuelewa ajenda ya maendeleo endelevu ya dunia na vipaumbele vyao wenyewe vya maendeleo huko Visiwani. Kampeni ya utoaji elimu kuhusu Malengo ya Dunia inalenga kuhakikisha kwamba vijana wanashiriki katika utekelezaji wake. Kampeni hiyo huko Pemba na Unguja ni mwendelezo wa juhudi zilizozinduliwa huko Arusha mwaka 2016 na Mratibu Mkazi wa

*Inaendelea ukurasa wa 16*

*Inatoka ukurasa wa 15*
Umoja wa Mataifa nchini Tanzania, Bw. Alvaro Rodriguez.

Akizungumza katika Shule ya Sekondari Lumumba, ambako moja kati ya vipindi vinne vya mafunzo yalitolewa, Ofisa wa Ushirika na Mawasiliano katika Ofisi ya Mratibu Mkazi alisema kwamba Ajenda ya Maendeleo Endelevu inahitaji ushiriki wa kila mmoja. Aliwapongeza wanafunzi kwa uelewa wao wa Malengo ya Dunia na hakikisho lao kwamba wanashiriki katika utekelezaji wake. Pia alionyesha umuhimu wa ushiriki wa vijana katika masuala ya maendeleo nchini Tanzania ambapo vijana wanaunda takribani asilimia 60 ya idadi ya watu.

“Kama vijana, mna dhima na wajibu muhimu kwa vijana wenzenu. Maarifa mliyopata leo yatawawezesha kuwa wajumbe hodari wa SDGs nyumbani, shuleni na katika jamii zenu. Kwa sababu hii, tunatumaini kwamba mtachukua wajibu wenu wa kuwa watetezi na watekelezaji wa shughuli zinazolenga kueneza na kutekeleza Malengo ya Dunia. Kwa hiyo, wajibu huo wa Malengo ya Dunia uko mikononi mwenu, hasa vijana,” alisema Bi. Didi, wakati akizungumza na vijana katika tukio hilo.

Mmoja wa washiriki, Bi. Lailat Mwinshehe kutoka Shule ya Sekondari Shamiani, alionyesha shukrani zake kwa mafunzo akieleza kwamba hiyo ilikuwa ni mara ya pili kwa mafunzo kama hayo kutolewa huko Pemba.“Najihisi kupata elimu, utambuzi na kuwezeshwa kuzungumzia kuhusu Malengo ya Dunia na familia yangu, marafiki zangu na wenzangu. Mwanzoni, maarifa haya hayakuwa bayana kwangu kwa sababu sikuwa nimepata fursa ya kushiriki mafunzo kama haya hapo kabla. Ajenda ya Malengo ya Dunia yatakamilika mwaka 2030, na wakati huo mimi nitakuwa na miaka 40. Nataka kuwa sehemu na shuhuda wa mafanikio katika utekelezaji wake, na ndio maana ninashiriki katika kutoa elimu miongoni mwa vijana wenzangu,” alisema Lailat.

Shule tatu za sekondari na kikundi cha waandishi wa habari ishirini walishiriki katika mafunzo huko Unguja, wakati ambapo zaidi ya wanafunzi 400 kutoka shule za sekondari Shamiani, Mitiulaya, Maendeleo na Limbani walipata mafunzo huko Chakechake, Pemba.

> *“Najihisi kupata elimu, utambuzi na kuwezeshwa kuzungumzia kuhusu Malengo ya Dunia na familia yangu, marafiki zangu na wenzangu. Mwanzoni, maarifa haya hayakuwa bayana kwangu kwa sababu sikuwa nimepata fursa ya kushiriki mafunzo kama haya hapo kabla. Ajenda ya Malengo ya Dunia yatakamilika mwaka 2030, na wakati huo mimi nitakuwa na miaka 40. Nataka kuwa sehemu na shuhuda wa mafanikio katika utekelezaji wake, na ndio maana ninashiriki katika kutoa elimu miongoni mwa vijana wenzangu,”*
>
> **- Ms. Lailat Mwinshehe, Mshiriki wa mafunzo ya maendeleo endelevu ya dunia.**

**Matukio Yajayo**

27 Januari – Siku ya Kimataifa ya Kuwakumbuka Waathirika wa Mauaji ya Halaiki

4 Februari – Siku ya Saratani Duniani

6 Februari – Siku ya Kimataifa ya Kukomesha Kabisa Ukeketaji Wanawake

20 Februari – Siku ya Dunia ya Haki za Kijamii

***Umoja wa Mataifa Madhubuti kwa Dunia Bora Zaidi !***



UNITED NATIONS TANZANIA

**UN Resident Coordinator’s Offce**

Communications Specialist

hoyce.temu@one.un.org

Phone: (+255) 22-219-5021

